


# Matatizo ya Masoko ya Mazao ya Wakulima







Warsha ya Nne ya

Wakulima wa Kanda ya Mashariki

Iliyofanyika Mjini Tanga,

Juni 2002

– SUA Project

# MATATIZO YA
# MASOKO YA MAZAO YA WAKULIMA

**Warsha ya Nne ya Wakulima wa**
**Kanda ya Mashariki**
**Iliyofanyika VETA Tanga**
**24-26 Juni 2002**

**Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya**
**kwa Wakulima**
**Wadogowadogo Tanzania**

***(TARP II-SUA Project)***

***JUNE 2002***

***Waandishi***

Bw. Razack O. Msangi
Dk. Joyce G. Lyimo-Macha

***Wahariri***

Wajumbe wa kamati ya utekelezaji wa Mradi

| | |
|---|---|
| Prof. L. D. B. Kinabo | Mratibu |
| Prof. R. E. Malimbwi | Mjumbe |
| Prof. E. K. Batamuzi | Mjumbe |
| Prof. A. J. Tarimo | Mjumbe |
| Dk. P. J. Makungu | Mjumbe |

**ISBN: 9987-605-66-4**

*Kimechapishwa na:*

Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP II-SUA Project)
Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo
SLP 3151
Chuo Kikuu, Morogoro
Simu: +255 23 2600970 au +255 23 2603511 ext. 4251

Toleo namba: TS 2-51

# Yaliyomo


**Dibaji** ........ **v**
**Vifupisho** ........ **vii**

**1. UTANGULIZI** ........ **1**
1.1. Maandalizi ya warsha ........ 1
1.2. Madhumuni ........ 1
1.3. Ufunguzi ........ 2
1.4. Kushirikishana wajibu ........ 2

**2. RATIBA** ........ **3**

**3. MBINU ZILIZOTUMIKA** ........ **3**

**4. KUBAINI MATATIZO YA MASOKO** ........ **4**
4.1. Makubaliano ........ 4
4.2. Kazi za vikundi ........ 4
4.2.1. Matatizo-wakulima ........ 5
4.2.2. Matatizo-Watafiti na Wagani/NGOs ........ 7
4.3. Tatizo kuu ........ 9

**5. MIKAKATI YA UTATUZI** ........ **11**
5.1. Mikakati-Wakulima ........ 12
5.2. Mikakati-Watafiti na Wagani/NGOs ........ 14

**6. MATAMKO MUHIMU** ........ **16**

**7. TATHMINI YA WARSHA** ........ **16**

**8. KUFUNGA WARSHA** ........ **18**

**9. VIAMBATANISHO** ........ **19**

Kiambatanisho Namba A: OrodhA ya washiriki ........ 19
Kiambatanisho Namba B: Matarajio na wasiwasi ........ 20
Kiambatanisho Namba C: Ratiba ........ 21
Kiambatanisho Namba D: Zoezi ........ 22
Kiambatanisho Namba E: Dirisha la johari ........ 23

# Dibaji

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo, kinatekeleza mradi wa Utafiti wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania. Mradi huu ambao ulianza rasmi Septemba 2000, unagharamiwa na Serikali ya Norway kupitia Shirika lake la Maendeleo (NORAD).

Kati ya shughuli muhimu zilizopangwa ili kutekeleza malengo ya mradi na pia kuimarisha uhusiano wa wakulima, watafiti na washauri wa wakulima ni kufanya warsha zenye madhumuni yafuatayo:

1. Kuwajumuisha watafiti, wakulima na washauri wa kilimo ili kudadisi kuhusu mambo muhimu yanayohitaji kushirikishwa pande zote kwa lengo la kufanikisha kilimo
2. Kuchambua na kuainisha matatizo yanayowakabili wakulima wadogowadogo
3. Kupanga ili kutambua mambo gani yapewe uzito au kipaumbele zaidi
4. Kushiriki katika kupeana uzoefu wa maeneo muhimu ya kilimo.

Chapisho hili linawasilisha mwenendo wa **Warsha ya Nne ya Wakulima wa Kanda ya Mashariki Kuhusu Matatizo ya Masoko ya Mazao ya Wakulima**, iliyofanyika katika ukumbi wa VETA, Tanga, tarehe 24-26 Juni 2002. Mwenendo wa warsha umechapishwa na kutolewa katika lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

L. D. B. Kinabo
Mratibu wa Mradi

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| COAS | Community Grassroot Initiatives Association *(Umoja wa Ushirikishwaji wa Jamii na Mipango)* |
| CBO | Community Based Organization *(Mashirika ya kijamii)* |
| MAFS | Ministry of Agriculture and Food Security *(Wizara ya Kilimo na Chakula)* |
| NGO | Non-Governmental Organization *(Shirika lisilo la Kiserikali).* |
| NLH | Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo. |
| SUA | Sokoine University of Agriculture *(Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo).* |
| TTCL | Tanzania Telecommunications Company Limited *(Shirika la Simu Tanzania)* |
| TARP II | Tanzania Agricutural Research Project Phase Two *(Mradi wa Taifa wa Utafiti wa Kilimo Awamu ya Pili)* |
| UNDP | United nations Development Programme *(Shirika la Umoja wa Mataifa la Mipango ya Maendeleo)* |



*Washiriki wa Warsha wakiwa kwenye picha ya pamoja*

# 1. UTANGULIZI

## 1.1. Maandalizi ya warsha, matarajio na wasiwasi wa washiriki

Warsha iliandaliwa na Mradi wa Uhakika wa Chakula na Pato la Kaya kwa Wakulima Wadogowadogo Tanzania (TARP II-SUA Project) unaotekelezwa na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Norway cha Kilimo (NLH) na Wizara ya Kilimo na Chakula (MAFS). Jumla ya washiriki 36 walihudhuria warsha hiyo ambayo ilifanyika katika Chuo cha VETA, Tanga. Washiriki 17 (ke 9 na me 8) walikuwa wakulima kutoka Wilaya za Morogoro, Lushoto, Kibaha, Muheza, Tanga, Handeni na Kilosa.

Washiriki watafiti 4 walitoka vituo vya Utafiti vya Ilonga, Kange, Mlingano na Tumbi, 6 walitoka SUA na mtafiti mmoja alitoka NLH, Norway. Jumla ya maafisa Ugani wanne (4) walishiriki, wawili kutoka Mikoa ya Tanga na Pwani na mmoja kutoka Mkoa wa Morogoro. Kadhalika washiriki wawili walitoka mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) na mmoja kutoka COAS Iringa ambae ndiye aliyekuwa mwezeshaji mkuu wa warsha (Kiambatanisho A)

Kwa vile mradi wa TARP II – SUA unalenga kuhakiki uhakika wa chakula na pato la kaya kwa wakulima wadogowadogo, warsha hii ilikuwa imewalenga takriban wadau wote wanaohusika na uzalishaji wa mazao mbalimbali hasa yale ya matunda na mbogamboga, mihogo, maziwa na bidhaa zake, iliki n.k. kutoka mikoa ya Morogoro, Pwani na Tanga. Kwa mawazo ya wanawarsha hao mradi wa TARP II-SUA umechukua jukumu hili la kuiendesha warsha hiyo ikiwa ni mkakati wake muafaka na msaada mkubwa kwa wakulima wadogowadogo katika kuielewa nadharia nzima ya soko huria pamoja na kubuni/kuona mbinu endelevu za kupambana na matatizo ya masoko ya mazao yalimwayo katika mikoa hiyo.

## 1.2. Madhumuni

Lengo kuu la warsha hiyo lilihusu kutazama kwa kina matatizo ya masoko ya mazao yanayolimwa na wakulima wa Mikoa tajwa na kung'amua njia (mbinu) mbalimbali ambazo zingeweza kusaidia kuyatatua matatizo hayo kikwelikweli. Kwa lengo hilo madhumuni mahususi ya warsha hiyo yalikuwa:

- Kubaini tatizo kuu (main problem) na matatizo mengine yaambatanayo na tatizo kuu la masoko ya mazao hayo.
- Kuainisha visababishi/viini (root causes) vya matatizo hayo
- Kufikia mbinu muafaka (zilizo ndani na nje ya uwezo wa wadau), kupendekeza wahusika wa utekelezaji wa mapendekezo hayo na kubaini manufaa kwa jamii endapo matatizo hayo yangetatuliwa.

### 1.3. *Ufunguzi wa warsha*

Mwenyekiti wa warsha Dk. (Bi) Joyce Lyimo-Macha aliwakaribisha washiriki na kueleza madhumuni ya warsha. Mwezeshaji aliwaomba washiriki kujitambulisha kila mmoja kwa kutaja jina lake, alikotoka, kitu kimoja akipendacho sana na kitu kimoja akichukiacho sana. Zoezi hili lilisaidia washiriki kujuana tabia vyema ikiwa ni msingi bora wa kuthaminiana kwa muda wote wa warsha.

Profesa Emmanuel Batamuzi, kwa niaba ya Mratibu wa mradi wa TARP II-SUA, aliwafahamisha washiriki pamoja na mgeni rasmi, malengo, madhumuni na shughuli za mradi kiujumla na kusisitiza matokeo (outputs) matano yanayotegemewa kupatikana kuwa ni:-

- Utafiti shirikishi wa wakulima wadogowadogo
- Kukuza uhusiano baina ya wakulima, watafiti na wagani
- Mafunzo ya shahada za juu kwa wafnyakazi wa MAFS
- Rasimu endelevu za namna ya kugharamia utafiti
- Tathmini ya matokeo ya tafiti mbalimbali

Baada ya hayo Profesa Batamuzi alimkaribisha mgeni rasmi, Mshauri wa Mifugo wa Mkoa wa Tanga Dk. Z. C. Lyimo, kufungua warsha.

Katika hotuba yake ya ufunguzi, mgeni rasmi aliwashukuru waandaaji wote waliowezesha warsha hii kufanyika hasa katika wakati huu ambapo uchumi wa nchi umetawaliwa na nguvu za soko na kwamba ilikuwa ni imani yake kuwa kwa ujumla matokeo ya majadiliano ya washiriki yangechangia katika kuweka misingi endelevu ya kuwasaidia wakulima na wafugaji wadogo wadogo katika Kanda ya Mashariki kuongeza kipato chao cha kaya na hivyo kupunguza umasikini.

### 1.4. *Kushirikishana wajibu (responsibility sharing)*

Mwezeshaji alishauri, na kukubaliana na washiriki kupanga na kufuata utaratibu ufuatao:-

#### 1.4.1. *Viongozi wa warsha*

Bi Estorode R. Mtangi alichaguliwa kwa kura nyingi kuwa Mwenyekiti wa warsha akisaidiwa na makatibu Elizabeth J. Msoka na Ndg. Kangure R. Misalaba. Jukumu la utunzaji muda lilishikwa na Bi. Nancy Kihara.

#### 1.4.2. *Kanuni*

Wanawarsha wote walipanga kanuni kuu zifuatazo ambazo zilifuatwa na kila mshiriki wa warsha kwa kadiri ilivyowezekana:

- Kutovuta sigara ukumbini/maeneo ya umma

- Wote kuzingatia na kutulia wakati wa kujadili mada
- Wote kujali na kuzingatia muda (muda ni mali)
- Wote kuthaminiana (kiumri, hoja, majibu, michango n.k.)
- Wote kuheshimiana (kiumri, hoja, majibu, michango n.k)
- Kuzingatia usafi wa mazingira
- Kutolewa pombe n.k. ukumbini na katika maeneo ya hadhara
- Kuchangia kwa uwezo wote na kwa uwazi
- Kuishi kama familia moja hadi mwisho wa warsha.

## 2. RATIBA

Kutokana na matarajio na wasiwasi wa washiriki kwenye warsha hiyo (Kiambatanisho B) ratiba ilipangwa kwa pamoja na majadiliano kuongozwa kukidhi madhumuni ya warsha yenyewe pamoja na kuongeza nguvu ya matarajio na kupunguza wasiwasi/hofu ya washiriki. Ratiba iliyokubalika na wote, ilikuwa na maeneo makuu sita yafuatayo:-

- Utangulizi, masuala ya awali na ufunguzi
- Kuelewana na kutofautisha maana ya soko, sokoni, ugani, soko huria, mkulima, utafiti
- Kubaini matatizo ya masoko ya mazao yalimwayo katika kanda ya Mashariki na viini (visababishi) vyake
- Majadiliano vikundini
- Mikakati ya utatuzi wa matatizo hayo, mapendekezo, wahusika wakuu wa utekelezaji na manufaa kwa jamii
- Tathmini ya warsha kila siku na warsha kwa ujumla

Takribani saa saba hadi nane na nusu zilitumika kila siku kwa kazi ya pamoja (ukumbini) na vikundini (Ratiba – Kiambatanisho C)

## 3. MBINU ZILIZOTUMIKA KUWEZESHA

Mbinu shirikishi zilitumika kwa kadiri ya uwezo wa kila mshiriki. Majadiliano yalifanyika katika vikundi vikubwa mchanganyiko, vikundi vidogo vidogo vilivyolenga watu/taaluma maalum (focus groups), kwa mfano kundi la akina mama wakulima peke yao, akina baba wakulima peke yao, watafiti peke yao na wagani peke yao. Mbinu nyingine zilizotumika zilikuwa pamoja na kutoa maelekezo mafupi (front short lectures), majadiliano ya pamoja, chemsha bongo (brainstorming), washiriki kubadilishana uzoefu wa mifano hai ya kukabiliana na matatizo husika, vibwagizo vya kuondoa ukimya (ice breaking exercises), michezo kadhaa ya kuongeza viwango vya ushirikishwaji ili kupanua ari ya kufikiri, kuchambua zaidi masuala mbalimbali pamoja na michoro iliyosaidia kueleweka kwa mada/hoja husika.

# 4. KUBAINI MATATIZO YA MASOKO YA MAZAO YA CHAKULA NA VISABABISHI VYAKE

## *4.1. Makubaliano/kuelewana pamoja juu ya maana ya maneno ya msingi – soko, sokoni, soko huria, kazi, ugani, utafiti, mkulima na tatizo*

Kwa kuwa haja ya kujua maana ya baadhi ya maneno hayo hapo juu ilijitokeza kwenye matarajio ya wana warsha, muda wa kutosha ulitumika kueleweshana maana ya maneno hayo kama ifuatavyo:

- **Soko** – lilikubalika kuwa ni taaluma inayohusu harakati au shughuli nzima za mzunguko wa bidhaa kutokea hifadhi, usafirishaji hadi uuzaji – (Soko ni fani/taaluma na sio mahali kama ilivyokuwa imefikiriwa na washiriki waliokuwa wengi).
- **Kazi** – kuwa ni shughuli yoyote halali inayompatia mtu riziki yake
- **Sokoni** – Ni mahali ambapo zipo bidhaa/mazao/huduma ambapo wanunuzi na wauzaji hubadilishana bidhaa/huduma hiyo, aidha kwa thamani watakayokubaliana.
- **Mkulima** – ni mtu yeyote anayetegemea riziki yake kutokana na mazao ya mimea au ya mifugo.
- **Ugani** – shughuli za ugani zilieleweka kuwa zinahusika na ushauri wa mara kwa mara wa shughuli za maendeleo. Kwa mantiki hiyo wapo maafisa ugani wa kilimo, maendeleo ya jamii, ushirika, elimu, mifugo n.k. na wataalamu hawa walielezwa kuwa wapo vijijini na ngazi ya kata.
- **Tatizo** (matatizo) – lilikubaliwa kuwa ni jambo/kitu chochote ambacho kinazuia. Maneno mbadala yaliyotajwa kulingana na maana hiyo ni pamoja na kigingi, kizingiti, kipingamizi au kizuizi
- **Soko huria** – lilieleweka kwa maneno kama kubabaisha, kutokuwa na uhakika, hali ya kuwepo kwa bei yoyote, hali ya kuuziana na kununua kwa bei ya maafikiano. Kimsingi washiriki waliliona soko huria kama ni sera mpya ambayo wakulima wadogo wadogo inabidi waifahamu vizuri ili waweze kuwa wakulima wafanya biashara. Hivyo soko huria walilielewa kuwa kumbe ni ushindani
- **Utafiti** – ulikubalika kuwa ni uchunguzi wa kina na mtiririko mzima wa kutafuta/kujua ukweli kisayansi.

## *4.2. Kazi vikundini ili kubaini matatizo na visababishi*

Washiriki walijigawa katika vikundi vinne; akina mama wakulima, akina baba wakulima, watafiti na wagani/NGOs. Vikundi hivyo vilitumia muda wa kutosha kubaini matatizo ya masoko ya mazao yalimwayo katika Mikoa hii hususani mboga, matunda, hiliki, mihogo n.k. Sababu za matatizo hayo vile vile zilibainishwa na kila kundi kuwasilisha matokeo ya kazi yake kama ifuatavyo:-

4.2.1. majibu ya kundi la Wakulima (makundi 2)

4.2.2. majibu ya kundi la Watafiti na wagani/NGOs (makundi 2)

## 4.2.1. MATATIZO YA MASOKO YA MAZAO NA VISABABISHI/VIINI VYAKE (BILA KUJALI KIPAUMBELE) – KUNDI LA WAKULIMA

| WAKULIMA WANAWAKE | | WAKULIMA WANAUME | |
|---|---|---|---|
| **MATATIZO -** Jinsi wanaki-kundi walivyobaini na kipaumbele | **Visababishi vikuu** | **MATATIZO -** Jinsi wanakikundi walivyobaini na kipaumbele | **Visababishi vikuu** |
| 1. **Ukosefu wa usawa wa kijinsia** (wanawake wanakosa muda kutafuta masoko ya bidhaa/maz ao kwa vile kazi nyingi zimewatinga) | • Mila na desturi potofu katika jamii<br>• Elimu haba ya maisha<br>• Kutokufahamu hali ya kileo. | 1. **Bei ndogo** | • Ubora finyu wa mazao/bidhaa<br>• Wakulima kukosa ushirikiano wa kuamua bei pamoja<br>• Barabara na madaraja mabovu /duni<br>• Mazao /bidhaa kutotangazwa<br>• Kuwa tegemezi wa zao moja (k.m. matunda au mboga tu)<br>• Ukosefu wa utaalamu wa usindikaji |
| 2. **Bei ndogo** | • Ufinyu wa ubora wa bidhaa zinazozali-shwa<br>• Kukosekana kwa utaratibu wa kuwa na bei maalum ya zao/bidhaa. | 2. **Ukosefu wa mshikamano/ushiriki ano wa wakulima /vikundi vya ushirika** | • Kukosekana kwa hamasa/elimu ya ushirika/ushirikiano<br>• Urasimu katika taratibu za kuanzisha ushirika<br>Mitaji duni/ masharti magumu ya mikopo |
| 3. **Ubovu wa miundo mbinu** -barabara mbovu -madaraja mabovu | • Ukosefu wa utaratibu wa kudumu wa kuzikarabati barabara na madaraja<br>• Wakulima kushindwa kukarabati barabara katika maeneo yao<br>• Uongozi ambao hauna mwamko wa kubuni mambo ya maendeleo. | 3. **Uzalishaji holela – kila mkulima au wengi wao kuzalisha zao hilo hilo au kuzalisha bila kulijua soko** | • Wakulima kukosa ushirikiano na mshikamano wa pamoja, pamoja na ukosefu wa elimu ya kilimo endelevu na stadi zihusuzo kilimo cha mzunguko wa mazao. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4. **Uzalishaji duni** | • Ukosefu wa pembejeo<br>• Kukosa utaalamu wa kutumia pembejeo mbadala<br>• Zana duni za uzalishaji<br>Mitaji midogo (hali duni ya uchumi) | | |
| 5. **Ukosefu wa habari za masoko na matumizi yake** | • Ukosefu wa mfumo wa utoaji habari za masoko hadi kwa mkulima mdogo<br>• Mikoa, Wilaya, Tarafa kata na wakulima wenyewe kutojitahidi kutafuta habari hizo.<br>Elimu ndogo ya wakulima ya uchambuzi wa habari zenyewe ili kuzitumia kwa wakati muafaka. | | |



*Kikundi cha wakulima wanawake wakiwa katika zoezi la kutambua visababishi vya matatizo ya masoko ya mazao*

## 4.2.2. MATATIZO YA MASOKO YA MAZAO NA VISABABISHI/VIINI VYAKE- KUNDI LA WATAFITI NA WAGANI

| WATAFITI | | WAGANI na NGOs | |
|---|---|---|---|
| **MATATIZO** - Jinsi wanaki-kundi walivyobaini na kipaumbele | **Visababishi vikuu** | **MATATIZO** - Jinsi wanaki-kundi walivyobaini na kipaumbele | **Visababishi vikuu** |
| **1. Bidhaa duni** | • Kutozingatia mbinu bora za kilimo<br>Mitaji/fedha kidogo za uendeshaji kilimo | **1. Ubora duni wa mazao** | Uwezo mdogo wa mkulima kupata na kununua pembejeo za kilimo kutokana na bei kubwa ya pembejeo na umbali wa huduma hiyo.<br>• Kukosa utaalamu wa usindikaji na hivyo mazao (matunda/mboga) kuoza haraka<br>• Wakulima kutozingatia ushauri wa kilimo utolewao na wagani. |
| **2. Kuzalisha kiholela bila kuzingatia/ kutafuta soko** | • Ukosefu wa mbinu/stadi husika<br>Wakulima kukosa mpango endelevu wa uzalishaji mazao kwa kugawana soko (i.e. kila mtu anazalisha mazao hayo hayo) | **2. Uduni wa elimu ya utafutaji wa masoko** | • Mawasiliano hafifu ya soko kati ya wakulima, wataalamu mbalimbali<br>• Elimu ndogo ya masoko kwa wagani |
| **3. Miundo mbinu isiyofaa** | • Serikali za ngazi zote kutoboresha miundo mbinu hiyo<br>• Ushiriki mdogo wa wananchi vijijini katika kuboresha miundo mbinu | **3. Ukosefu/ubovu wa miundo mbinu** | • Serikali na uongozi wa ngazi mbalimbali kutowajibika ipasavyo<br>• Wakulima/wananchi wenyewe kutochangia nguvu zao katika kukarabati barabara hata pale wanapokuwa na uwezo huo. |
| **4. Mbinu duni za usindikaji wa mazao** | • Elimu ndogo kuhusu usindikaji wa mazao<br>• Huduma ndogo za ugani (uwezo na mbinu za usindikaji hawanazo)<br>• Mitaji midogo ya kuwekeza katika ununuzi wa vifaa | **4. Bei ndogo ya mazao/bidhaa** | • Wakulima kutokuwa na umoja wao hivyo kukosa nguvu ya ushindani (kukosa uwezo wa kupanga bei yao na vipimo au viwango vyao) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **5. Ukosefu wa vikundi vya wakulima** | • Ukosefu wa hamasa vijijini<br>• Historia mbaya iliyopita ya vyama vya ushirika<br>• Ubinafsi wa wakulima wachache "kubakia hivyo (conservative) bila sababu za msingi" | **5. Kutotangaza bidhaa zetu na kukosa utamaduni wa kutumia (kupenda) bidhaa zetu** | • Kukosa utaalamu wa utangazaji na kutojua wapi panafaa kutangaza bidhaa husika<br>• Ukosefu wa desturi za kutumia bidhaa zetu<br>Mila potofu (kasumba!) |
| **6. Kutojitangaza kibiashara** | • Ukosefu wa elimu ya masoko na utangazaji<br>• Kukosa fedha za kuwezesha matangazo/ mawasiliano (gharama kubwa) | | |
| **7. Kutopenda bidhaa zetu wenyewe** | • Kasumba kuwa bidhaa za nje ni bora zaidi kuliko za ndani | | |

### 4.3. *Kubaini tatizo kuu na maeneo ya kumsaidia mkulima*

Baada ya kila kikundi kumaliza kuwasilisha, kutetea/kuongeza yale yaliyolenga kuboresha yaliyowasilishwa, takribani washiriki wote walieleza kuanza kuona uwezekano mkubwa wa kuweza kutatua baadhi ya matatizo ya masoko ya mazao yao, kwani ufumbuzi wa matatizo hayo yalikuwa yanajionyesha vizuri zaidi.

Kwa sababu hiyo basi mwezeshaji alichangia na kufanya majumuisho ya matatizo husika kwa ujumla:

***Kwamba:***

**Tatizo kuu la masoko ya mazao ya wakulima wa kanda ya mashariki lilionekana kuwa ni ukosefu wa elimu (ufahamu wa kileo) ili kuuona na kukubali ukweli na kubadilika. Ukosefu wa ufahamu huo umewafanya wakulima kutojua mbinu za jinsi soko huria linavyofanya kazi na kushindwa kwao kujipanga (organize) pamoja ili kutatua matatizo yao ya uzalishaji na upatikanaji wa masoko endelevu.** Kwa sababu hiyo wakulima/wazalishaji wadogo wadogo wa mazao mbalimbali wanakosa mfumo wao wa pamoja na uamuzi wa pamoja wa kupanga bei ya mazao yao na wanashindwa kupata taaluma za usindikaji n.k. Hali hii ya wakulima kutoona pamoja, inawafanya wapangiwe bei isiyolipa gharama zao za uzalishaji, wauziwe pembejeo na madawa yasiyofaa na hivyo kushindwa kuwa wafanyabiashara wanaotazamiwa kwenye mfumo wa soko huria.

Matokeo ya hali na uhusiano huo ni mkulima kuendelea kuathirika katika:-

- ***Imani potofu*** – Kuamini mambo yasiyofaa (uchawi); kutopenda kutumia bidhaa zetu wenyewe, kukataa kuona ukweli wa hali ya sasa n.k.
- ***Bei ndogo*** – ya mazao yake huendelea kuwa ndogo ikilinganishwa na gharama za uzalishaji (aghalabu wakulima wengi hawazijui gharama zao za uzalishaji). Wakati huo huo bei za zana, madawa na pembejeo za kilimo ni kubwa.
- ***Ubora finyu wa mazao***- Ubora wa mazao yenyewe ni wa chini na dawa na pembejeo zitumikazo zipo chini ya viwango, japo ni ghali pia.
- ***Sera/sheria*** – Baadhi ya sera na sheria zilizopo hazimlindi mkulima mdogo mdogo. Kodi kadha wa kadha zimeambata mazao husika na utaratibu uliokusudiwa kurahisisha maendeleo/kukua kwa soko huria unawekewa ukiritimba/vikwazo. Wawekezaji hawajapata mvuto wa kuwekeza vya kutosha kwenye sekta ya kilimo pamoja na usindikaji wa mazao ya mboga na matunda.
- ***Ukosefu wa usawa wa kijinsia*** – Wanawake kutumia muda wao mwingi katika kuzihudumia familia na kukosa muda wa

kutafuta masoko ya mazao, kuboresha uzalishaji, kuhudhuria mikutano ya elimu mbalimbali au vyote n.k.

- ***Ubovu wa miundo mbinu*** – Jukumu la kudumisha barabara za vijijini kupitika kwa urahisi wakati wote bado linahitaji juhudi kubwa. Wakulima wangeweza kutengeneza maeneo wanayomudu ili kurahisisha usafirishaji wa mazao yao; lakini bado majukumu makubwa ya kazi hii ni ya Halmashauri za Wilaya na Serikali Kuu.
- ***Ukosefu na uduni wa matumizi ya habari za masoko*** – Ni vyema jitihada zikafanyika kupanua huduma hizi kutoka kitengo kinachohusika Makao Makuu ya Wizara ya Ushirika na Masoko, kuja Mikoani hadi Wilayani n.k. Vivyo hivyo Maafisa Ugani husika wa Mikoa na Wilaya wangeweza kuanzisha mifumo ya taarifa za bei za mazao "marketing information systems" (MIS) yao msimu kwa msimu Kimkoa, Kiwilaya, Kikata n.k.
- ***Kukosa soko la uhakika na uzalishaji duni*** – Haya yote ni matokeo ya matumizi ya mbegu duni, mbolea "feki", matumizi ya zana duni za kilimo, kutotumia utaalamu wa kilimo, kutotumia kilimo cha mzunguko, hifadhi mbovu ya mazingira (mmomonyoko wa udongo) n.k.
- ***Wakulima kutokuwa na mifumo yao*** – Mifumo hiyo ikiundwa na kuendelezwa itasaidia kupanga bei ya mazao ya kikundi/wakulima husika, kuweka viwango muafaka vya vipimo (ujazo/uzito), na kuendeshwa na uongozi wao wa pamoja na kufanya uamuzi wao wa pamoja. Kwa vile mtazamo wa wakulima hawa huwa ni wa kibiashara, vikundi hivi hugeuka baadaye kuwa vya wakulima wafanyabiashara; (Mifano ya "Producer Marketing Groups" PMGs – ya COAS – Iringa na Umoja / ushirika wa uzalishaji wa mboga na matunda Lushoto (UBIRI) n.k. vilitajwa kama vyombo vinavyotatua matatizo ya wakulima)
- ***Ukosefu wa mitaji*** – Kukosa namna ya kujipanga ili waanzishe mifuko yao ya ndani (kutoa malipo ya awali ya mazao yao, ununuzi wa pembejeo n.k.)
- ***Kutofahamika/kutotangazika vyema kwa bidhaa/mazao husika***
- ***Uongozi mbovu*** – Viongozi mbalimbali kutokuwa wabunifu kimaendeleo na kutotaka kuamsha ari ya kujitolea (Harambee) kwa maendeleo ya jamii. Katika maeneo mengi kuna "BORA VIONGOZI" badala ya "VIONGOZI BORA".

Wanawarsha walikubaliana kuanza kujenga tabia ya kubadilika, kusaidiana, kushikamana na kujali usawa wa kijinsia katika utatuzi wa matatizo mbalimbali yanayowakabili ikiwa ni pamoja na tatizo la kuboresha mbinu za upatikanaji wa masoko ya mazao yao.

Kadhalika maeneo yafuatayo yalibainishwa na kukubalika na wanawarsha kuwa ndiyo maeneo makuu ya kumsaidia mkulima:-

- Wasaidiwe kupata elimu (utaalamu) wa kusindika mboga na matunda na na kufunga bidhaa (packaging)
- Wasaidiwe kujengewa uwezo wa kuwa na mifumo yao (organisational skills) na kufikia uamuzi - (lini, vipi, kiasi na ubora wa kuuza)
- Wasaidiwe kutambua njia mbalimbali za kuboresha masoko yao - kwa mfano wawezeshwe kuelewa mfumo wa soko huria unavyofanya kazi (warsha hii ikiwa njia sahihi ya kuianza kazi hiyo)
- Wasaidiwe/wasaidiane kupata wanunuzi wa mazao/bidhaa mbalimbali
- Wasaidiwe kudumisha miundo mbinu - barabara bora, hifadhi ya mazao n.k.
- Wasaidiwe kubuni na kukuza mitaji endelevu
- Wasaidiwe kupata na kutumia habari za masoko pamoja na kubaini mazao mbadala kufuatana na hali halisi ya soko

## 5.0. KUTAFUTA/KUBAINI MIKAKATI YA UTATUZI WA MATATIZO NA KUASHIRIA WAHUSIKA

Wanawarsha walijigawa katika makundi makuu manne (4) ya Wagani/NGOs; Watafiti na Wakulima (ke na me) (makundi 2), ili kupanga mikakati husika, kuashiria watekelezaji na kubaini manufaa yatakayopatikana kwa jamii kwa ujumla kama matatizo hayo yangetatuliwa. (Kwa mchanganuo husika tafadhali angalia vipengele 5.1 na 5.2 vya taarifa hii).

## 5.1. MIKAKATI/MAPENDEKEZO YA KUTATUA MATATIZO HUSIKA, WAHUSIKA WAKUU NA MANUFAA KWA JAMII KUNDI LA WAKULIMA KWA UJUMLA WAO

| | TATIZO | MIKAKATI/MAPENDEKEZO YA KUKABILIANA NA TATIZO | WAHUSIKA WAKUU | MANUFAA KWA JAMII |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Bei ndogo** | - Kujiunga katika vikundi na kupanga bei ya pamoja<br>- Kuwa wadadisi wa bei ya mazao<br>- Kuongeza ubora wa mazao/ bidhaa | Wakulima/Wagani | -Kuboresha kipato cha kaya (familia)<br>-Jamii kuelimika na kushirikiana<br>-Kupunguza umasikini |
| 2 | **Imani potofu** | - Kuielimisha jamii, k.m. kujua athari kwa kiumbe kitakachozaliwa na mama ambaye "kanyimwa" kula mayai katika ujauzito wake? | Mgani, NGOs, Dini, Afya, Halmashauri za Wilaya, Serikali za ngazi zote. | - Kuona (visualize) vizuri zaidi<br>- Kuelimika – kuona hali halisi (ukweli uliopo)<br>- Muda mwingi sasa kutumika katika shughuli za uzalishaji /maendeleo Jamii kupendana, kusaidiana na kuaminiana |
| 3 | **Uzalishaji duni** | - Kuanzisha mitaji ya kuzalisha mali<br>- Kutumia utaalamu, kutumia pembejeo mbadala m.f. (mboji, samadi na kutumia kanuni bora za kilimo na ufugaji n.k.) | Mkulima, Mgani, Mtafiti, NGOs | - Kupunguza umasikini, kupanua ajira na kuongeza kipato cha kaya |
| 4 | **Kukosa mbinu za usindikaji** | - Mafunzo husika yapatikane<br>- Vifaa husika na mitaji viwezeshwe | Mkulima, Mgani, Mtafiti, Serikali za ngazi zote, SUA, NGOs | - Kujiinua kimapato, lishe bora<br>- Kupunguza umasikini<br>- Kushirikishana taaluma (usindikaji) |
| 5 | **Uduni wa elimu** (ufahamu usiopevuka) | - Mafunzo kwa vikundi vitakavyo undwa na vilivyopo kwenye mpango<br>- Kuchapisha/na kusoma vipeperushi<br>- Matangazo kwa njia ya redio, TV, magazeti n.k.<br>- Ziara za mafunzo | Wagani, Watafiti, Serikali, NGOs, wafadhili, Dini. | - Jamii kuhimili barabara mbinu za uzalishaji, masoko na ulaji<br>- Kupunguza umasikini<br>- Kuwa wabunifu na kufanya kazi kwa bidii |
| 6 | **Ukosefu wa ubunifu** | - Mikutano, ziara za mafunzo, makongamano semina n.k.<br>- Wakulima kuungana pamoja (kuchangia mawazo mbalimbali) | Wakulima, Wagani, Halmashauri za Wilaya, NGOs, wafadhili | - Kujiendeleza<br>- Kupata ajira<br>- Kupunguza umasikini |

| | TATIZO | MIKAKATI/MAPENDEKEZO YA KUKABILIANA NA TATIZO | WAHUSIKA WAKUU | MANUFAA KWA JAMII |
|---|---|---|---|---|
| 7 | **Ukosefu wa habari za masoko na matumizi yake** | - Kudadisi habari za masoko<br>- Kupeana habari | Mkulima, Mgani, Serikali kuu, wafadhili. | - Kujiajiri<br>- Kuongeza vipato vya kaya /jamii<br>- Kupunguza umasikini |
| 8 | **Ukosefu wa usawa wa kijinsia** | - Wanawake kutafuta/kuelewa haki zao<br>- Muda mwingi utumike kuwaelimisha wanaume na wanawake kwa pamoja, ikiwezekana wanaume wafundishwe zaidi maswala ya jinsia kuliko wanawake.<br>- Kufanya kazi zote kwa kushirikishana isipokuwa zile maalum kwa kundi maalum. | Wakulima, Viongozi wa dini, Serikali za ngazi zote, NGOs/CBOS. | -Kuondokana na mila potofu<br>-Kuongeza kiwango cha uzalishaji katika kaya na kipato<br>-Kila mtu kujishughulisha ipasavyo<br>-Kutendeana haki na kujenga taifa lenye kuthaminiana<br>-Kupunguza umasikini |
| 9 | **Uzalishaji holela** | - Kuunda vikundi vidogo vidogo vya uzalishaji mali kwa kuzingatia soko (mahitaji) | Wakulima, Wagani | -Kupunguza umasikini<br>-Mgawano wa kazi kisayansi |
| 10 | **Ubora hafifu wa mazao/bidhaa** | - Upatikanaji wa pembejeo bora<br>- Kufuata kanuni bora za kilimo | Wakulima, Wagani, Watafiti, NGOs | -Kupata bei kubwa hivyo kuongeza kipato na kuboresha maisha ya kaya |
| 11 | **Ubovu wa miundo mbinu** | - Kuwa na utaratibu wa kudumu wa matengenezo | Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya, Wakulima | -Kurahishisha mawasiliano; usafirishaji wenye ufanisi zaidi wa watu na mazao/bidhaa<br>-Kupunguza gharama zauzalishaji |
| 12 | **Sera/vikwazo/ sheria zisizo-mlinda mkulima mdogo** | - Sera mbalimbali kurejewa ili zimsaidie mkulima zaidi<br>- Vikwazo ambavyo havina ulazima viondolewe<br>- Wakulima/washirikishwe kikamilifu kwenye masuala yote yanayowahusu<br>- Wakulima wajionyeshe kuwa wapo WAFURUKUTE | Serikali Kuu, Halmashauri za Wilaya, Serikali za vijiji, Wakulima, Wagani, Watafiti | -Kuwa na vipato /shughuli ambazo zinatekelezeka na endelevu<br>-Kupanua ufahamu wa mambo muhimu katika maisha ya kila siku (hasa kwa wakulima) |
| 13 | **Uongozi usio bora (ukosefu wa misingi bora ya uongozi)** | - Kuwahamasisha viongozi hao waweze kudumisha utawala bora na kuwa wabunifu wa shughuli za maendeleo katika maeneo husika<br>- Kuendeleza/kufufua harambee/kujitegemea | Serikali za ngazi zote, wakulima, Jamii, NGOs | -Jamii kuwa wazalendo wa nchi yao na kukereketwa katika shughuli za maendeleo<br>-Kuongeza kipato kutokana na wafanya- biashara kufika maeneo ambayo huwa ni vigumu sana kufikika kwani barabara zitatengenezwa (harambee!) |

## 5.2. MIKAKATI/MAPENDEKEZO YA KUTATUA MATATIZO HUSIKA, WAHUSIKA WAKUU NA MANUFAA KWA JAMII KUNDI LA WATAFITI, WAGANI NA NGOs KWA UJUMLA WAO

| | TATIZO | MIKAKATI/MAPENDEKEZO YA KUKABILIANA NA TATIZO | WAHUSIKA WAKUU | MANUFAA KWA JAMII |
|---|---|---|---|---|
| 1 | **Bei ndogo** | - Kuunda vikundi/umoja wa wakulima (Ushirika)<br>- Kusindika mazao<br>- Kuongeza ubora wa mazao<br>- Wakulima kujua/ kutunza gharama za uzalishaji | Wakulima, Wagani, Viongozi wa vijiji, Watafiti | - Bei nzuri ya mazao na kuongeza uwezo wa ushindani kibiashara |
| 2 | **Imani potofu** | - Elimu kwa jamii | Wagani, Serikali zote, Jamii (wakulima) | -Mabadiliko ya jamii katika uzalishaji na matumizi bora ya rasilimali ikiwa ni pamoja na muda. |
| 3 | **Uzalishaji duni** | - Elimu ya kilimo bora iwezeshwe na kufuatwa<br>- Pembejeo zipatikane karibu na wakulima na wakulima wawe na uwezo wa kuzinunua (kuhudumia/kugharamia kilimo chao)<br>- Kuunda vikundi vya akiba na mikopo<br>- Mikopo yenye riba nafuu ipatikane | Wakulima, Wagani, Mashirika ya mikopo, NGOs, Serikali za ngazi zote hasa Halmashauri za Wilaya | - Kuongezeka kwa uzalishaji na bidhaa, mazao bora |
| 4 | **Ukosefu wa mbinu za usindikaji** | - Elimu ya usindikaji ipatikane<br>- Kuwepo vyanzo vya mtaji (Akiba na mikopo, mikopo n.k.)<br>- Kuwepo vikundi vya wakulima vinavyosindika na kutawanya huo uzoefu/ujuzi kwa wengine | SUA, Wagani, NGOs, Watafiti, SIDO/UNDP /CBOS, Wakulima | -Kuongeza thamani ya bidhaa<br>-Kupanua soko la ndani na nje<br>-Kupunguza upotevu wa mazao<br>-Kumrahisishia mlaji (ale bidhaa iliyokamilika) ili atumie muda wake zaidi kwa uzalishaji |
| 5 | **Uduni wa elimu ya masoko na uzalishaji, n.k** | - Wakulima na wahusika wengine wapate elimu juu ya uzalishaji na masoko<br>- Wadau waimarishe mawasiliano | Wakulima, Wagani, Watafiti, Taasisi za kibiashara, Serikali za ngazi zote, NGOs/CBOs | -Uhakika wa uzalishaji na uuzaji<br>-Elimu bora ya kilimo kwa jamii |

| | TATIZO | MIKAKATI/MAPENDEKEZO YA KUKABILIANA NA TATIZO | WAHUSIKA WAKUU | MANUFAA KWA JAMII |
|---|---|---|---|---|
| 6 | **Ubora finyu** | -Matumizi ya mbinu bora za uzalishaji pamoja na taaluma ya "vifungashi" (packaging) | Serikali Kuu, Halma- shauri za Wilaya, NGOs, Wagani, Wakulima, Watafiti | -Kuzalisha bidhaa bora -Ongezeko la pato kutokana na bei nzuri itakayorudisha gharama za uzalishaji na ziada |
| 7 | **Uzalishaji holela usiozingatia soko** | -Kutoa na kutafuta elimu ya masoko -Kuanzisha vikundi vya uzalishaji vitakavyozingatia mahitaji ya soko | Wakulima, Wagani, NGOs Viongozi wa vijiji, Watafiti | -Uzalishaji wa mpangilio -Kudumu/ uhakika wa masoko |
| 8 | **Ukosefu wa habari za masoko na uwezo mdogo wa kutumia habari hizo** | -Kutangaza bidhaa zinazozalishwa ili watu wawe na habari nazo -Kuimarisha mawasiliano kati ya vijiji, miji na masoko -Kuanzisha vituo vya utoaji habari ngazi za Taifa hadi Wilayani | Watafiti, Wagani, Wakulima, Serikali Kuu (Wizara husika), Serikali /Mitaa. NGOs/ TTCL/ CBOs | -Uhakika wa masoko na bei nzuri unaolenga mahitaji halisi na ubora unaotakiwa |
| 9 | **Ukosefu wa usawa wa kijinsia** | -Kazi (isipokuwa zile maalum za kimaumbile) zifanywe kwa usawa -Elimu ya jinsia kwa jamii hasa wanaume na jinsia zote | Mashirika ya Dini, NGOs/CBOs, Wagani, Wakulima (jamii), Wagani/Watafiti, Serikali za ngazi zote | -Ushiriki mkubwa wa jinsia zote katika uzalishaji na shughuli za maendeleo -Kuboreka kwa mawazo,uamuzi unaozingatia hoja za wote na hivyo kujenga jamii pevu na yenye mapenzi namshikamano mkubwa |
| 10 | **Ubovu wa miundo mbinu** | - Ushirikishaji wa wanavijiji katika kuboresha miundo mbinu Serikali za ngazi zote kuwa na mpango wa kudumu wa kuboresha miundo mbinu hasa barabara, madaraja vijijini | Wananchi, Uongozi wa ngazi zote, Serikali kuu, za wilaya, NGOs/CBOs, Wafadhili | -Urahisi wa kufikisha bidhaa /mazao sokoni kwa wakati muafaka -Kupatikana kwa pembejeo na zana zingine za kilimo kwa wakati muafaka |
| 11 | **Sera, sheria, vikwazo visivyo na manufaa kwa mkulima mdogo** | -Kutoa elimu na kuwajibika -Vikwazo vya kunufaisha upande mmoja viondolewe -Kodi/ushuru kwa mkulima mdogo ziondolewe -Sheria/sera zilizopo zitazamwe ili zimlinde mkulima na kumpa uwezo mkubwa wa kufanya biashara ndani ya "soko huru" | Serikali Kuu, Serikali za Wilaya, Vijiji, Wizara husika, Wakulima kuboresha mikusanyiko yao (farmers forums) | -Ushindani wa haki wa shughuli za kilimo na biashara -Kuendeleza uhuru unaodhamiriwa katika ushindani ndani ya mfumo wa soko huria. |

## 6. MATAMKO MUHIMU YA WARSHA

1. Warsha ilitamka kuwa matokeo ya kazi ya warsha hii ya kuchambua matatizo ya masoko ya mazao ya wakulima kanda ya Mashariki iwafikie Watendaji Wakuu wa Wizara za Kilimo na Chakula, Ushirika na Masoko, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa hatua za utekelezaji. Aidha, vikwazo/vizuizi vilivyopo vinavyomzuia mkulima kuuza mazao yake ya ziada kwa mfumo wa soko huria kivitendo vilegezwe, vipunguzwe na kuondolewa kabisa pale itakapobidi.
2. Serikali isimamie kwa karibu zaidi mikakati ya kuondoa umasikini na kumwendeleza mkulima mdogo mdogo ambaye ndiye mtoa mchango mkuu wa uchumi wa nchi yetu.
3. Akina mama wasikilizwe katika ngazi zote ili washiriki na kutoa mawazo yao na uamuzi katika masuala yote ya maendeleo katika kaya zao, jamii na Taifa kwa ujumla.
4. Warsha kama hizi zitumike na Serikali na wadau wengine ili kupata maoni ya wakulima, wananchi wakati wa kuandaa sera na mikakati inayowagusa katika maisha yao ya kila siku.
5. Jitihada zichukuliwe ili hapo baadaye warsha nyingine kama hii ifanyike kwa ajili ya kupima utekelezaji.

## 7. TATHMINI YA WARSHA

Tathimini ya warsha ilifanyika kwa kila mshiriki kuandika maoni yake katika kadi tatu, moja akieleza ni imani gani ameijenga baada ya kuja, kuona, kusikia na kushiriki katika warsha hii. Kadi ya pili, mambo ambayo hayakumridhisha na maoni ya namna ya kuyaboresha na ya tatu, juu ya maandalizi na mbinu zilizotumika katika uwezeshaji (Jedwali 7.1).

## 7.1. TATHMINI YA WARSHA

| Fungu kubwa (Cluster NO.) | SWALI LA KWANZA<br>Baada ya Warsha Imani iliyojengeka (Clustered opinions) (Maoni) | Idadi ya washiriki |
|---|---|---|
| 1 | Sasa naamini hakuna kisichowezekana chini ya jua, usichokijua mwenzio anakijua, ujinga ndio chanzo kikuu cha umasikini, kushirikiana na kuchangiana mawazo ndiyo suluhisho la kujikwamua na umasikini, kila mmoja akitimiza wajibu wake (mikakati tuliyojiwekea) umasikini utapungua, wakulima wanaweza kuanza wao kwanza kutatua matatizo yao ya masoko ya bidhaa/mazao yao n.k. | 19 |
| 2 | Nitakuwa mwalimu mzuri kwa wenzangu, tupange na kutatua matatizo yetu ya masoko ya mazao pamoja, kwa asilimia 65 naweza kuelimisha wenzangu, mbinu za kujitegemea katika kutatua matatizo ya masoko ya mazao ya wakulima, ni muhimu kutumia juhudi na maarifa na kuwa wakweli ( wa kuiona hali halisi ya mambo) ili kutoka katika nyumba ya umasikini, uwezo wa kuhamasisha wenzangu umeongezeka, inawezekana kubadilika (kimaendeleo) n.k. | 11 |
| 3 | Mahusiano kati ya wagani, watafiti, serikali, NGOs na wakulima yataboreka na kusaidiana katika kutatua matatizo ya masoko ya mazao ya wakulima na ya uzalishaji duni. Warsha kama hizi ni nzuri kumpatia mwananchi (mkulima) wa kawaida habari na elimu ya yale yanayomzunguka, ili aongeze kipato chake na kupanua mwanya (uwezekano) mkubwa uliopo wa masoko, usindikaji, n.k. Haki za kijinsia zimefahamika. | 10 |

| Fungu kubwa (Cluster NO.) | SWALI LA PILI<br>Ambayo hayakuniridhisha na namna ya kuboresha (Clustered opinions) | Idadi ya washiriki |
|---|---|---|
| 1. | Yote yalifurahisha, hakuna sababu za msingi za kutofurahishwa na yote tuliyojifunza, kwani ufunuo zaidi wa mambo umepatikana n.k. | 16 |
| 2. | <u>Yasiyofurahisha:</u><br>-Kuchelewa kufika kwa baadhi ya wanakikundi (1)<br>-Wanawake wasiotambua haki zao hadi leo na huku vyombo vyote vya habari (TV, magazeti n.k.) vinaimba kila siku (1)<br>-Uhafifu wa mapokezi Veta (4), ratiba ya warsha kutotolewa mapema (1)<br>-Wanawarsha wengine kutochangia mawazo yao (3), kutozingatia muda/kanuni zetu (2), washiriki wengine kuongea sana na kupiga porojo (2) n.k. | Jumla ya washiriki 14 walieleza |
| 3. | <u>Maoni/mapendekezo</u><br>Vyeti vya kushiriki vitolewe (3); vitini vitolewe baada ya mafunzo (1); washiriki waje na bidhaa wanazotengeneza ili iwe ni changamoto na kuonyesha juhudi zao katika ubunifu (1); muda uongezwe (4); tarehe za kufika zilitofautiana (ziwe moja sasa) (3); wakulima wengi zaidi washirikishwe (3); wafugaji nao washirikishwe (1); idadi ya wanawake iongezwe (1); washiriki wakae sehemu moja ili wabadilishane mawazo na uzoefu (1); wadau wengine washirikishwe - mashirika ya dini na wauzaji wa pembejeo (3) n.k. | Jumla ya washiriki 17 walitoa mapendekezo/ushauri wao. |

| Fungu kubwa (Cluster NO.) | SWALI LA TATU<br>Maoni kuhusu maandalizi na mbinu zilizotumika katika uwezeshaji (Clustered opinions) | Idadi ya washiriki |
|---|---|---|
| 1. | Maandalizi ni mazuri/mazuri sana ila mahudhurio pungufu. Mbinu za uwezeshaji ni nzuri/nzuri sana ni za kitaalamu, mwezeshaji anajua kazi yake, mbinu zimewezesha kila mtu aelewe, ziwepo picha za video kulingana na masomo, kuwepo na ufuatiliaji baada ya mafunzo (kongamano) ili kupima utekelezaji, mbinu za uwezeshaji ni nzuri mno ni shirikishi na zimetia hamasa, SUA/watafiti watembelee vijijini kutoa ushauri/matokeo ya utafiti wao, wawezeshaji walitakiwa walipie gharama lakini mradi umewasaidia senti za kujikimu vile vile (shukrani), mbinu zilizotumika kuwezesha ziendelee. | 24 |

## 8. KUFUNGA WARSHA

Warsha ilifungwa rasmi na Mkuu wa Wilaya ya Tanga k.n.y Mkuu wa Mkoa wa Tanga Capt. George Mkuchika. Mgeni rasmi alisisitiza kuhusu umuhimu wa masoko ya mazao na teknolojia ya kuhifadhi na kusindika mazao kabla ya kuyapatia masoko ndani na nje ya nchi. Pamoja na ufungaji huo, washindi wa mashindano ya wakulima, wataalamu wa ugani na watafiti katika kanda ya mashariki walitunukiwa zawadi (vyeti vya utendaji bora na fedha taslimu).

# 9. VIAMBATANISHO

**(KIAMBATANISHO A)**

## ORODHA YA WASHIRIKI

| Na. | Jina | Jinsia | kazi | Kijiji | Kata | Anuani |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Baraka Wabeya | Me | Mk | Mkata | Mkata | SLP 200 Handeni, Tanga |
| 2. | Yusufu Kome | Me | Mk | Vibaoni | Vibaoni | SLP 200 Handeni, Tanga |
| 3. | Asha Mwinshehe | Ke | Mk | Matuli | Ngerengere | SLP 28 Ngerengere |
| 4. | Nuru Juma | Ke | Mk | Pangani | Tumbi | SLP 30021 Kibaha |
| 5. | Mohamed Bakari | Me | Mk | Dochi | Lushoto | SLP 3 Lushoto |
| 6. | Asha kassim | Ke | Mk | Kwalei | Mamba | SLP 50 Soni |
| 7. | Lucas Shemndolwa | Me | Mk | Maringo | Malindi | SLP 2 Lushoto |
| 8. | Cosmas Kidebe | Me | Mk | Matuli | Ngerengere | SLP 28 Ngerengere |
| 9. | Estrode Mtangi | Ke | Mk | Dochi | Dochi | SLP 262 Lushoto |
| 10. | Sabina Masilamba | Ke | Mk | Pangani | Tumbi | SLP 30021 Kibaha |
| 11. | Shomari Swago | Me | Mk | Matuli | Ngerengere | SLP 28 Ngerengere |
| 12. | Yohana jeremia | Me | Mk | Lushoto | Lushoto | SLP 72 Lushoto |
| 13. | Susan Pentzel | Ke | Mk | Maringo | Malindi | SLP 2 Lushoto |
| 14. | Wallace Mbwana | Me | Mk | Semgano | Kilulu | SLP 174 Muheza |
| 15. | Magreth Salim | Ke | Mk | Mindu | Mkuzi | SLP 477 Muheza |
| 16. | Mwanaisha Hatibu | Ke | Mk | Kwemsala | Kilulu | SLP 25 Muheza |
| 17. | Cleophas Mutabuzi | Me | Mk | Mlalo | Misalai | SLP 5707 Bulwa Est.Tanga |
| 18. | Hamisi Shekimweri | Me | Mga | Kideleko | Vibaoni | SLP 200 Handeni, Tanga |
| 19. | Elizabeth Msoka | Ke | Mga | Lushoto | Lushoto | SLP 72 Lushoto |
| 20. | Jeremia Kapera | Me | Mga | Ngerengere | Ngerengere | SLP 747 Morogoro |
| 21. | Nancy Kihara | Ke | Mga | Mkoani | Kibaha | SLP 30153 Kibaha |
| 22. | Fulgence Mishili | Me | Mtaf | SUA | SUA | SLP 3007 Morogoro |
| 23. | Adrian B. C. Mbiza | Me | Mtaf | Ilonga | Ilonga | SLP Ilonga, Kilosa |
| 24. | John Msemo | Me | Mtaf | Tumbi | Tumbi | SLP 30031 Kibaha |
| 25. | Kungure Misalaba | Me | AUs | Amani | Tanga | SLP 178 Tanga |
| 26. | Peter Mbangulila | Me | ABi | Tanga | Tanga | SLP 5095 Tanga |
| 27. | Pius Kavana | Me | Mtaf | Kange | Kange | SLP 5016 Tanga |
| 28. | Ernest Bwedo | Me | NGO | Majengo | Muheza | SLP 5479 Tanga |
| 29. | Grete Benjaminsen | Ke | Mtaf | As Norway | As Norway | SLP 5001 NLH1432 Norway |
| 30. | Dismas Mwaseba | Me | Mtaf | SUA | SUA | SLP 3000 Morogoro |
| 31. | Rogers Malimbwi | Me | Mtaf | SUA | SUA | SLP 3013 Morogoro |
| 32. | Akwilini Tarimo | Me | Mtaf | SUA | SUA | SLP 3005 Morogoro |
| 33. | Emanuel Batamuzi | Me | Mtaf | SUA | SUA | SLP 3020 Morogoro |
| 34. | Adolf Nyaki | Me | Mtaf | Mlingano | Mlingano | SLP 5088 Tanga |
| 35. | Joyce Lyimo-Macha | Ke | Mtaf | SUA | SUA | SLP 3044 Morogoro |
| 36. | Razack Msangi | Me | Mwe | Iringa | Iringa | SLP 664 Iringa |

**Me**=Mwanamme; **Ke**= Mwanamke; **Mk**= Mkulima; **Mga**= Mtaalamu wa Ugani;
**Mtaf**= Mtafiti; **AUs**= Afisa ushirika (W); **ABi**= Afisa Biashara (W); **Mwe**= Mwezeshaji.

**(KIAMBATANISHO B)**

## MATARAJIO NA WASIWASI YA WASHIRIKI KAMA YALIVYOONYESHWA SIKU YA KWANZA TAREHE 24-06-2002

| Na. | MATARAJIO (Maelezo yanayofanana/kuhusiana yameainishwa pamoja - "clustered") | Idadi ya wahusika |
|---|---|---|
| 1 | Matatizo ya mazao/bidhaa za wakulima kanda ya Mashariki yatafahamika wazi na mapendekezo/mikakati ya ufumbuzi kutolewa/ kupatikana: kwa kubadilishana uzoefu mbalimbali; kwa kuona umuhimu wa kukuza uhusiano kati ya wakulima; watafiti na wagani, kujifunza mbinu mbalimbali za kutatua matatizo ya masoko ya mazao ya wakulima; kukubaliana viwango bora vya uzalishaji ili kupata masoko ya uhakika zaidi; kupata mwanga zaidi wa kuboresha masoko ya bidhaa/mazao nje na ndani ya nchi; kurudi na ujuzi mbalimbali wa kuwasaidia wenzetu huko vijijini katika utatuzi wa matatizo kadha wa kadha ikiwa ni pamoja na yale ya uzalishaji duni na ukosefu wa masoko; kujua mbinu za kuwa mkulima mfanyabiashara (kumudu soko huria); n.k. | 22 |
| 2 | Kujua mbinu za kujitegemea katika kufuta umasikini; jinsi ya kushirikiana katika kutatua matatizo ya masoko ya mazao; kupata uzoefu wa wakulima katika kupokea matokeo ya tafiti mbalimbali; kuwa na maisha mazuri katika kaya; kufahamiana; kuelimika kiujumla n.k. | 9 |

| Na. | WASIWASI/HOFU (Maelezo yanayofanana/kuhusiana yameainishwa pamoja - "clustered") | Idadi ya wahusika |
|---|---|---|
| 1 | Je matatizo na ufumbuzi wa sababu za ukosefu wa masoko ya mazao ya kilimo na mifugo katika kanda ya Mashariki yatapatikana? (tutaweza kweli?); tutakuwa wawazi na wakweli kuyabaini matatizo hayo?; Je wanawarsha hawatatoa maazimio au mapendekezo ambayo hayatekelezeki?; Na hivyo kutotatua tatizo la msingi/kuu?; Mabadiliko ya mara kwa mara ya sera za nchi zitaathiri bidhaa zitokanazo na kilimo; n.k. | 7 |
| 2 | Hakuna wasiwasi wowote | 5 |
| 3 | Muda hautatosha | 4 |
| 4 | Utaratibu wa ufuatiliaji baada ya mafunzo utakuwepo/utakuaje? Wataalamu wasije kutumia lugha ngumu kama kiingereza; huenda baadhi ya wanasemina wakashindwa kuelewa elimu ya uuzaji wa bidhaa nje; wanasemina huenda wakawa wasahaulifu wa yale yatakayokuwa yamefundishwa katika semina; n.k. | 4 |
| 5 | Namna ya kupata misaada/mikopo vikundini; je masoko yakiimarika wakulima watakumbuka kujiwekea akiba?; Wakulima wanaelewa ukweli wa matatizo ya masoko ya mazao yao?; n.k. | 3 |

**(KIAMBATANISHO C)**

## RATIBA

### Mwongozaji –Mwezeshaji Mkuu, Wawakilishi wa Mradi na Mwenyekiti wa Warsha

| SAA | SIKU YA 1 | SIKU YA 2 | SIKU YA 3 |
|---|---|---|---|
| 2:30 asubuhi – 4:30 | • UTANGULIZI, MAMBO YA AWALI NA UFUNGUZI<br>• KUGAWANA MAJUKUMU (Viongozi)<br>• KANUNI ZETU<br>• MATARAJIO NA WASIWASI<br>• KUPANGA RATIBA | • TAARIFA FUPI MAMBO MUHIMU TULIYOJIFUNZA SIKU YA 1<br>• Mawasilisho ya matatizo kuendelea (vikundi 4) | • Mambo muhimu ya siku ya 1-2 (tumejifunza nini hadi sasa)<br>• Mapendekezo, wahusika wakuu na manufaa kwa jamii (vikundini) |
| | C | H A | I |
| 5:00 – 7:00 | • KUBAINI MATATIZO YA MASOKO YA MAZAO NA MIFUGO<br>- Kukubaliana maana ya maneno muhimu, Soko, Sokoni, Soko huria, utafiti, ugani na kazi<br>- Kazi vikundini | • Majadiliano kukubaliana matatizo<br>• Kubaini tatizo kuu | • Kuendelea kuwasilisha mikakati n.k.<br>• Kujadiliana<br>• Kufikia muafaka wa mikakati, wahusika wakuu na manufaa<br>• Tathmini ya warsha |
| | CHAKULA | CHA | MCHANA |
| 8:30 – 10:30 | - Kazi vikundini<br>- Kuanza kuwasilisha (matatizo) (vikundi 4)<br>- Je umejisikiaje leo? | • Kazi vikundini kuweka mikakati, kupendekeza wahusika na kubaini manufaa kwa jamii<br>• Je umejisikiaje leo? | • Kufunga warsha |

**(KIAMBATANISHO D)**

(1) ZOEZI LA HESABU YA UMOJA -(Lengo 1 jawabu 1)


***Maelezo*** - Kama wakulima wakishirikiana (wakishikamana) wakawa na dhamira moja, wakajipangia utaratibu (mfumo wao) wa kutatua matatizo yao – siku zote watapata majawabu yaliyo SAWA au yanayofanana mfano; wa hizi namba 621, 532 na 853 zimetolewa na kujumlishwa (kufuata utaratibu fulani, nidhamu maalum) na kupata jawabu moja la 1089

| | | |
|---|---|---|
| 621 | 532 | 853 |
| -126 | -235 | -358 |
| 495 | 297 | 495 |
| +594 | +792 | +594 |
| 1089 | 1089 | 1089 |

**Jibu moja wote = 1089.**

(2) UTATU WA KUBORESHA UHUSIANO (TARP II-SUA Project)

***Maelezo*** - Kujenga na kuboresha mahusiano kati kati ya wakulima, wagani na watafiti siku zote KUTAZAA mahusiano mapya, kuona kupya (new vision) ubunifu mpya, uzalishaji wa kutosha na hivyo kuongeza kasi ya maendeleo, uhakika wa chakula katika kaya utakuwepo na sekta ya kilimo na mifugo itaboreka kwa ujumla wake. Tuanze na kuiendeleza hii safari kwa kuvunja gamba la ubinafsi linalotutawala.




Hatua ya kwanza ya kuanza safari, ni kila mtu mshiriki/mdau wa Mradi wa TARP II-SUA atoke ndani mwake awezeshwe kutoka na kusema yanayomsibu na kupendekeza utatuzi (solutions) Wengi wanaushukuru Mradi kwa hilo-hii ni pamoja na sisi COAS. Kimsingi hakuna sababu za mradi huu kutofanikiwa – kutotoa matokeo (outputs) yaliyotegemewa. Kama zitakuwepo basi zitafahamika kisayansi.

**(KIAMBATANISHO E)**

## (1) TUJITAMBUE SOTE - (DIRISHA LA JOHARI)

***Maelezo***

Kila mtu ni kama fumbo lenye sehemu moja iliyo wazi na sehemu nyingine ambayo imefichika. Zoezi hili la dirisha la Johari (lililotungwa na Joe Luft na Harry Ingham) linatusaidia kuelewa jinsi ya kukua katika kujifahamu, na jinsi ya kujenga kuaminiana katika timu za watu na jamii tunamoishi kwa kushirikishana na kupeana mshindo nyuma au kukosoana. Wakulima, watafiti na wagani sote tunaweza kupanua sehemu yetu ya "UHURU" kwa kupunguza ukubwa wa sehemu za "UPOFU", "GIZA" NA "ILIYOJIFICHA" ili tujenge mahusiano bora, ya wazi na ya kweli wakati wote.

***Kielelezo cha Dirisha la Johari***

| | Inayojulikana Kwa mwenyewe | Isiyojulikana kwa mwenyewe |
|---|---|---|
| Inayojulikana kwa wengine | **HURU**<br>- unaifahamu wewe<br>- wengine wanaifahamu | **KIPOFU**<br>(huijui)<br>(mshindo nyuma) |
| | Kushirikishana | (kufunua/kufumba_ |
| Isiyojulikana kwa wengine | **ILIYOFICHIKA**<br>-haijulikani na wengine (wewe tu) | **GIZA**<br>(akiba) |

**(2) NYUSO MBILI (NJIA MBALIMBALI ZA KUANGALIA MATATIZO)**

(Picha yenyewe yenye nyuso mbili haikuambatanishwa humu lakini nakala za kutosha ziligawanywa kwa washiriki na ufafanuzi kutolewa)

***Lengo*** – Lengo la zoezi hilo lilikuwa kuwafanya washiriki wa kongamano hilo kutambua njia mbalimbali za kukabiliana na matatizo kwa kushirikishana/kuonyeshana. Njia hii itawasaidia/iliwasaidia kutambua matatizo yao na kuyarekebisha, na kujenga hali ya mahusiano mazuri katika kikundi (jamii) ili waanze kushughulikia tatizo moja baada ya jingine kutegemeana na uzito wa tatizo na hali ya mahali.